# COLLEGE OF YOUTH EDUCATION IN TANZANIA (CoYETa)
# AND
# MWANZA YOUTH CENTRE (M.Y.C)

**P.O.BOX 11836 MLANGO MMOJA AREA MWANZA -TANZANIA**

**TEL:+255(028)2540305, +255 753 188 061, FAX: +255(028)2540305,**

**Email: info@coyeta.ac.tz, Website: www.coyeta.ac.tz**


**NAMBA ZA USAJILI WA CHUO:** VETA NI **VET/MZA/PR/2012/C/055**
TEWW NI **IAE/OS/0152**
BASATA NI **BST/5109**

# FOMU YA MAELEZO YA KUJIUNGA NA KOZI YA UTALII, HOTELI NA USAFIRI WA ANGA (TOURISM, HOTEL & AIRLINE MANAGEMENT) KWA MWAKA WA MASOMO 2025/2026



Mkuu wa Chuo anayo furaha kubwa kukuarifu ndugu, ____________________________________, kwamba umechaguliwa kujiunga na Masomo ya **KOZI YA UTALII/USAFIRI WA ANGA/HOTELI** katika chuo cha Mwanza Youth Centre kwa mwaka 2024. Hivyo, unapaswa kusoma, kuelewa na kuyafuata maelekezo yaliyo kwenye fomu hii.

***NB: PAMOJA NA KOZI YA UTALII,USAFIRI WA ANGA NA HOTELI, CHUO KINATOA KOZI NYINGINE MBALIMBALI KAMA MAABARA (LABORATORY ASSISTANT), UHAZILI (SECRETARIAL), B.O.A (BUSINESS OPERATION ASSISTANT), MUZIKI, KINGEREZA NA KIFARANSA, COMPUTER APPLICATIONS NA MAINTENANCE. HIVYO, CHUO KINAKUPA FURSA YA KUBADILISHA KOZI NA KUSOMA KOZI NYINGINE YOYOTE INAYOTOLEWA NA CHUO CHETU KULINGANA NA MAHITAJI YAKO.***

## 1.0. TAREHE YA KUWASILI NA KUSAJILI

Unatakiwa kuripoti chuoni tarehe ________________________. Chuo chetu kipo Jijini Mwanza maeneo ya Mlango mmoja, Jengo la Vijana.

## 2.0. MATAKWA YA KUSAJILIWA

Wanafunzi wote waliochaguliwa watafanyiwa usajili baada ya kutimiza yafuatayo:

### A) MALIPO YA ADA

Hakuna mwanafunzi ambaye atafanyiwa usajili au ataruhusiwa kuingia darasani bila kulipa Ada inayostahili.

**Mgawanyo wa Ada ni Kama Ifuatavyo:**

| **Jina la Kozi** | **Utalii/Usafiri wa Anga/Hoteli** |
|---|---|
| **Kitu Kinacholipiwa** | **Kiasi (Tshs)** |
| Ada ya Kozi | 740,000 |
| Fomu | 10,000 |
| Kitambulisho | 5,000 |
| Ada ya Mtihani | 25,000 |
| Serikali ya Wanafunzi | 5,000 |
| Huduma ya Kwanza | 5,000 |
| Maendeleo | 10,000 |
| Sheria za chuo (students bylaw) | 3,000 |
| **Jumla Kuu** | **803,000** |

**Awamu Za Kulipa**

| **S/N** | **AWAMU** | **MWEZI WA KULIPA** | **KIASI CHA KULIPA KWA AWAMU** |
|---|---|---|---|
| 1 | AWAMU YA KWANZA | Siku ya kuripoti | 300,000/= |
| 2 | AWAMU YA PILI | Baada ya miezi 2 | 200,000/= |
| 3 | AWAMU YA TATU | Baada ya miezi 2 | 200,000/= |
| 4 | AWAMU YA NNE | Baada ya miezi 2 | 103,000/= |
| **Jumla** | | | **803,000/=** |

**NAMNA YA KULIPA**

i) Ada yote iliyoelezwa hapo juu italipwa katika Benki ya Benki ya CRDB kwenye Akaunti nambari **0150355105000** kwa jina la **COYETA.**
ii) Mwanafunzi anapaswa kuwasilisha Nakala Halisi ya Malipo (Original Bank Pay in Slmp) kwenye ofisi ya Uhasibu Chuoni. Hundi, Keshi, na aina nyingine za malipo hazitapokelewa.
iii) Ada haitarudishwa kama mwanafunzi amesitisha masomo au ameacha chuo.

**B) PICHA (PASSPORT SIZE)**
Mwanafunzi anatakiwa kuja na picha mbili za passport, moja kwa ajili ya kitambulisho cha shule na nyingine kwa ajili ya matumizi ya ofisi.

**C) KARATASI YA RIMU (REAM PAPER)**
Mwanafunzi anatakiwa kuja na pakti moja ya karatasi nyeupe ya rimu isiyo na mistari yoyote (one packet of plain Ream paper) kwa ajili ya matumizi ya ofisi, itakayotumika katika shughuli zote za ku mhudumia kielimu kwa mwaka mzima.

## 3.0. NYARAKA ZA MHIMU KWA AJILI YA USAJILI

i) Kwa wanafunzi wote waliochaguliwa wanatakiwa kuja na vyeti halisi vya shule, nakala za matokeo, na cheti cha kuzaliwa (kama anacho).
ii) Hakutakuwa na ubadilishaji wa majina yaliyopo kwenye vyeti vitakavyokuwa vimewasilishwa wakati wa zoezi la usajili isipokuwa imesemwa vinginevyo.

## 4.0. HUDUMA YA MALAZI, CHAKULA, NA MATIBABU

i) Chuo kina hosteli nzuri na za kisasa kwa wanafunzi wa mbali au wanaohitaji. Gharama za hostel ni shilingi laki mbili na elfu hamsini (Tshs 250,000/=) kwa mwaka, fedha hii italipwa kwa awamu tatu. Gharama hizo zinajumuisha chumba, kitanda, godoro, umeme na maji. Ada ya Bweni ilipwe katika nambari ya akaunti ya Benki ya EQUITY **3005211899015**,yenye jina "**MWANZA YOUTH CENTRE**"
ii) Chuo hakitoi chakula kwa wanafunzi, hata hivyo kuna huduma nyingi za vyakula za watu binafsi maeneo ya karibu na chuo kwa gharama nafuu kabisa.

## 5.0. SARE

Sare zinapatikana chuoni kwa gharama ya **tshs 70,000/=,** ambayo pia inalipiwa kupitia nambari ya akaunti ya Benki ya EQUITY **3005211899015**, yenye jina "**MWANZA YOUTH CENTRE**".

## 6.0. MCHANGO WA MAHAFALI

Kwa mwanachuo mhitimu atachangia kiasi cha **Tshs 50,000** kama gharama za Joho la Mahafali katika mwaka wake wa kuhitimu. Kwa mwanachuo asiye mhitimu atachangia kiasi cha **tshs 10,000** kama mchango wa Mahafali. Fedha zote hizi zilipwe kupitia nambari ya akaunti ya Benki ya EQUITY **3005211899015**, yenye jina "**MWANZA YOUTH CENTRE**" kufikia tarehe 30 mwezi Juni ya mwaka husika.

## 7.0. MAWASILIANO

Wanafunzi waliosajiriwa chuoni kwetu wanapaswa kutembelea mara kwa mara mbao za matangazo na tovuti yetu kwa ajili ya kupata taarifa mbalimbali za kitaaluma na mambo mengine ya kijamii kama ratiba za masomo, matokeo ya mitihani, semina, n.k

## 8.0. NIDHAMU

Wanafunzi wote wanatakiwa kuonesha tabia njema ndani na nje ya maeneo ya chuo, hii ikiwa ni pamoja na kufuata sheria na taratibu zote za chuo. Kushindwa kufanya hivyo, kutasababisha mhusika kuchukuliwa hatua za kinidhamu ambazo zinaweza kuwa ni pamoja na kufukuzwa chuo.

**IMETOLEWA NA:**
Ev. Emmanuel Mambo (Mkuu wa Chuo)

**KARIBU SANA MYC UFANIKIWE KIELIMU, KIROHO NA KIMWILI**
**Kwa Msaada Zaidi Piga kwenye Namba 0753188061/0756481887**